

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UGONJWA ULIOTOKEA KAGERA

Dar Es Salaam, 21 Machi, 2023.

Ndugu Wananchi, itakumbukwa kuwa mnamo tarehe 16 Machi 2023, Wizara ya Afya ilitoa taarifa ya uwepo wa watu wenye dalili za homa, kutapika, kutokwa damu maeneo mbalimbali ya mwili na figo kushindwa kufanya kazi, katika kata za Maruku na Kanyangereko, Halmashauri ya Bukoba Vijijini, Mkoa wa Kagera.

Ndugu Wananchi, uchunguzi uliofanywa katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii (National Public Health Laboratory) umethibitisha uwepo wa **virusi vya Marburg**, ambavyo vinasababisha ugonjwa unaojulikana kama **Marburg Viral Disease (MVD)**. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), Ugonjwa huu uligunduliwa kwa mara ya kwanza nchini Ujerumani mwaka 1967 katika mji wa Marburg na ndio asili ya jina lake, na umeshawahi kuripotwa katika nchi mbalimbali za Afrika na Ulaya.

Ndugu Wananchi Ugonjwa huu huambukizwa kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine hususan kwa njia ya kugusa majimaji (mfano; mate, mkojo, damu, machozi au kinyesi) yatokayo kwa maiti au mgonjwa mwenye dalili. Aidha, maambukizi yanaweza kutokea pia kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu iwapo mtu atakula au kugusa mizoga au wanyama walioambukizwa. **Dalili za ugonjwa** huu ni homa, kuumwa kichwa, maumivu ya misuli, kuishiwa nguvu, kutapika na kuharisha, kutoka damu sehemu za wazi za mwili n.k. Ugonjwa huu hauna tiba mahususi isipokuwa hutibiwa kwa dalili anazokuwa nazo mgonjwa.

Ndugu Wananchi, hadi kufikia siku ya leo tarehe 21 Machi, 2023, ikiwa ni siku tano tangu kuripotwa kwa watu wenye dalili nilizozitaja hapo juu, **jumla ya watu waliothibitika kuwa na ugonjwa huu ni nane (8) na kati yao, vifo ni vitano (5)**. Wagonjwa watatu (3) wanaendelea na matibabu katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoandaliwa Mkoani Kagera. Kwa niaba ya Serikali ninatoa pole kwa wote waliofiwa na ndugu, jamaa na marafiki kutokana na ugonjwa huu.

Handwritten signature

Ndugu Wananchi, nichukue fursa hii kuwatoa hofu kuwa hadi sasa Serikali imefanikiwa kudhibiti kasi ya maambukizi mapya ya ugonjwa huu. Hadi sasa ugonjwa huu haujatoka nje ya eneo lililoripotiwa, yaani katika Halmashauri ya Bukoba, mkoani Kagera. Aidha, watu waliotangamana na wagonjwa au wahisiwa wanafuatiwa kwa karibu na wataalamu wa afya (contact tracing). Nitumie fursa hii kuwashukuru Uongozi na watumishi wa afya hususani walio mstari wa mbele mkoani Kagera ambao wanaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuwahudumia wagonjwa na kuhakikisha ugonjwa huu unadhibitiwa. Vilevile ninaishukuru Timu ya Wataalamu kutoka Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuungana na timu ya Mkoa wa Kagera kukabiliana na ugonjwa huu kwa wakati.

Ndugu wananchi, Kipekee niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Kagera kwa kutoa ushirikiano kwa Serikali ikiwemo kutoa taarifa kuhusu tetesi za Ugonjwa huu. Niendeleo kuwaomba Wananchi kuchukua tahadhari za kujikinga dhidi ya Ugonjwa huu pamoja na magonjwa mengine ya kuambukiza kama inavyoshauriwa na wataalamu wa afya. Pia ninatoa rai kwa wananchi kutoa Taarifa kwa Serikali endapo kuna tetesi za mhasiwa au mtu mwenye dalili za ugonjwa huu. Aidha endapo kuna mtu yoyote mwenye dalili za ugonjwa huu afike kituo cha kutoa huduma za afya kwa ajili ya Uchunguzi na Matibabu.

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, ninatoa Wito kwa watumishi wa afya kote nchini kuzingatia Miongozo na Taratibu za Kuzuia na Kudhibiti Maambukizi (Infection Prevention and Control) wakati wote wa kutoa huduma kwa wananchi. Ninawasihii wananchi kutoa ushirikiano kwa wataalamu wa afya.

Imetolewa na;



Ummu A. Mwalimu (Mb.)

WAZIRI WA AFYA